**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA TATU

**08 NOVEMBA, 2018**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 08 NOVEMBA, 2018

**I. DUA:**

**II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**III. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**29. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Watumishi wa Umma walioajiriwa mwaka 2012 hawajapandishwa madaraja mpaka leo hii:-

Je, ni lini Watumishi hao watapandishwa madaraja.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 30. MHESHIMIWA LAMECK OKAMBO AIRO (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Eneo la Rorya lina ukubwa wa kilomita za miraba 9345, eneo la ziwa likiwa ni asilimia 78. Nchi kavu ni asilimia 22 na shughuli kubwa zinazofanyika katika eneo hili ni Uvuvi, Kilimo, Ufugaji na Biashara, idadi ya watu katika eneo hilo ni takribani 400,000 (Sensa mwaka 2012) hadi sasa Wilaya inategemea na kutumia Gereza la Wilaya ya Tarime ambalo linahudumia wahalifu wote wa Rorya na Tarime hasa ikizingatiwa kuwa shughuli zinazofanywa kwenye maeneo haya zinahusisha pia majirani zetu kutoka Uganda, Kenya n.k hivyo uhalifu kutokea kwa wingi ni jambo lisiloweza kuzuilika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Gereza Wilaya ya Rorya**.**

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

### 31. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete, ina upungufu wa Madaktari Bingwa na Wauguzi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Wataalamu hao katika Hospitali hiyo.

**32. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kumekuwa na ongezeko kubwa la Wagonjwa wa Kisukari nchini, aidha baadhi ya Watoto wanazaliwa wakiwa na ugonjwa huo:-

Je, Serikali ipo tayari kufanya uchunguzi na kueleza chanzo cha ugonjwa huo.

**33. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- wako Watoto wengi wametelekezwa na Wazazi wao na kuachwa wakizagaa mitaani:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kuihamasisha Jamii kuwaasili watoto hao ili nao wafaidike na malezi ya Jamii.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**34. MHESHIMIWA JOSEPHINE THABITHA CHAGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Mhe. Rais alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kahama kupitia Nyangholongo, Bukwimba, Karumwa Nyijundu, Busolwa, Ngoma hadi Busisi Kivukoni kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

**35. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Mwaka 2015 akiwa katika Kampeni, Mhe. Rais aliwaahidi Wananchi wa Mji Mdogo wa Chala kuwa barabara ya lami iliyokuwa inajengwa ingepita nje ya Mji huo na hakuna nyumba ambayo ingevunjwa, lakini katika ujenzi barabara hiyo ilipita katikati ya Mji ilipokua inapita barabara ya vumbi na hivi karibuni Meneja wa TANROADS Mkoa wa Rukwa ametoa *notice* ya kuvunja nyumba za Wananchi zilizowekwa alama ya X:-

(a) Je, kwa nini Serikali inatoa kauli mbili tofauti kwa Wananchi;

(b) Je, Meneja wa TANROADS kutotekeleza ahadi hiyo ya Mhe. Rais inatafsiri gani kwa Wananchi wa Chala ambao Mhe. Rais aliahidi nyumba zao kutovunjwa.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**36. MHESHIMIWA LATHIFAH HASSAN CHANDE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wananchi wa Mkoa wa Lindi wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa muda mrefu hadi kusababisha baadhi ya Wananchi hasa wa Vijijini kutumia maji ya Mito na Mabwawa pamoja na Mifugo:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi mbalimbali ya maji Mkoani Lindi;

(b) Je, ni lini Serikali itahakikisha upatikanaji wa maji safi katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi ili kuepusha uwezekano wa magonjwa ya mlipuko kwa Wauguzi na Wagonjwa.

**37. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Vijiji vya Zanzui, Malita, Mwabujiku, Dodoma, Buyubi na Ikungulyasubi kwa muda mrefu viko kwenye mpango wa kupatiwa maji kutoka kwenye Bwawa la Zanzui linalotoa maji kwa Mji wa Maswa:-

Je, ni lini mpango huo utakamilishwa na Serikali ili Wananchi katika Vijiji hivyo wapate maji ya uhakika.

**38. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji ya bomba katika Mamlaka ya Mji mdogo Rujewa Wilayani Mbarali ni wa zamani hivyo haukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa:-

(a) Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kupanua mradi huo;

(b) Chujio la maji katika eneo la Mtaa wa Igomelo kwa sasa halitumiki kwa kuwa liko chini ya kiwango; Je, Serikali imechukua hatua gani kwa Wahandisi waliotoa michoro na kusababisha hasara ya fedha za Serikali

na Wananchi wakiendelea kupata shida ya maji katika Mji Mdogo wa Rujewa na hasa maeneo ya Igawa.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**08 NOVEMBA, 2018** **KATIBU WA BUNGE**